



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)



TANGAZO

NAFASI ZA UHAMISHO KWA WATUMISHI WA UMMA

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimeanzishwa mwaka 1997 kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania kiwe "Taasisi kuu ya Serikali ya kuratibu, kuhimiza, kukuza na kuwezesha uwekezaji nchini Tanzania na kuishauri Serikali kuhusu sera ya uwekezaji na masuala yanayohusiana na uwekezaji nchini. Kituo kinapenda kuwatangaza nafasi za kuhamia kwa watumishi wa umma ambazo zinategemewa kujazwa katika Ofisi za TIC Dodoma, Mwanza, Mbeya, Njombe, na Arusha.

Waombaji wenye sifa stahiki kwa mujibu wa Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi (Miundo ya Utumishi) kwa kada husika na wenye nia ya kufanya kazi katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) wanashauriwa kuomba nafasi zilizo wazi kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo;

NAFASI ZA KUJAZA KWA NJIA YA UHAMISHO KATIKA KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)

Na.	CHEO/KADA	IDADI YA NAFASI
1.	Afisa TEHAMA Mkuu I	1
2.	Afisa Uwekezaji Mkuu I	2
3.	Afisa Ukaguzi wa Ndani Mwandamizi I	1
4.	Afisa Sheria Mwandamizi I	1
5.	Afisa Uwekezaji Mwandamizi I	1
6.	Afisa Uwekezaji Mwandamizi II	1
7.	Afisa Ugavi Mwandamizi I	1
8.	Afisa Utumishi Mwandamizi I	1
9.	Mhasibu Mwandamizi I	1
10.	Afisa Tawala I	1
11.	Afisa Tawala II	1
12.	Afisa Uwekezaji I	4

13.	Afisa Uwekezaji II	1
14.	Msaidizi Kumbukumbu I	1
15.	Katibu Mahsusi I	3
16.	Msaidizi wa Kumbukumbu I	1
17.	Mwandishi Mwendesha Ofisi II	1
18.	Afisa Mahusiano I	1
19.	Mhasibu I	1
20.	Msaidizi wa Hesabu Mwandamizi I	1
	JUMLA	26

VIGEZO VYA KUHAMIA/MUOMBAJI

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania;
2. Uwe Mwajiriwa wa Serikali mwenye sifa stahiki kwa nafasi husika;
3. Barua ya maombi ipitishwe na Mwajiri wako na igongwe muhuri;
4. Maombi yote yaambatane na vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita; kwa wale waliofikia kiwango hicho, vyeti vya taaluma, na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali na vilivyothibitishwa (certified as true copies);
5. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika;
6. Muombaji athibitishwe utayari wa kujigharamia uhamisho huo;
7. Muombaji aweke Check Na. / Namba ya Ajira kwenye barua ya maombi;
8. Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, Hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA;
9. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 Januari, 2025.

Maombi yote yaandikwe na kutumwa kwa: -

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
Jengo la Manispaa ya Zamani-Sabasaba,
S.L.P. 2875,

DODOMA

Limetolewa tarehe
31 Desemba, 2024